

JINA: NAMBARI:

SHULE: TAREHE:

SAHIHI:.....

102/2

KISWAHILI

LUGHA

KARATASI YA PILI

JULAI / AGOSTI 2014

MUDA: SAA 2½

MTIHANI WA MWIGO WA WILAYA YA KURIA MASHARIKI 2014

Cheti cha Kuhitimu Masomo ya Kidato cha Nne Nchini Kenya

KISWAHILI

LUGHA

KARATASI YA PILI

MUDA: 2½

MAAGIZO

1. Andika **jina lako** na **nambari yako** katika nafasi zilizoachwa hapo juu.
2. **Tia sahihi** yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi zilizoachwa hapo juu.
3. Jibu maswali **yote**.
4. Andika **majibu** yako katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu cha maswali.
5. **Hakikisha** ya kwamba maswali yote yamo.

Swali	Upeo	Alama
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
JUMLA	80	

1. UFAHAMU (ALAMA 15)

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.

Tsunami, tetemeko la ardhi baharini iliyotokea Decemba mwaka wa 2004 katika bara la Asia ilikuwa na athari kubwa sana. Watu wasiopungua 170,000 walipoteza maisha yao kutokana na mawimbi yaliyotifuliwa na tsunami hiyo katika Bahari ya Hindi. Madhara ya maafa hayo yalitanda hadi maeneo ya mbali kama upwa wa Afrika Mashariki ulio na umbali wa takriban kilomita 7,000 kutoka kitovu kikuu cha tsunami hiyo. Janga hii limeibua mjadala kuhusu madhara yanayotokana na nguvu za kimaumbile. Nguvu za kimaumbile zina uwezo wa kuzua majanga yasiyoweza kutarajiwani. Mlima wa volkeno uliotulia unaweza kuvuvumuka kutapakaza zaha ambayo inaweza kuua maelfu ya watu kama ilivyotokea huko nchini Kongo.

Majanga ya kimaumbile huweza kusababisha maafa, misiba na tanzia isiyokuwa na mshabaha. Sio rahisi kuweza kutawasiri akilini kiwango cha madhara ya majanga haya hadi yanapotokea. Baadhi ya majanga ya kimaumbile ni kama vimbunga vya vumbi, zilizazla, mafuriko, tufani, radi, ukame na hata moto.

Licha ya kuwa binadamu hawana uwezo wa kuzuia kutokea kwake, zipo hatua ambazo zinaweza kuchukuliwa. Kwa mfano, yapo maeneo ambapo kutokana na historia ni rahisi kujua yapi ambayo huweza kutokea. Kuna maeneo ambapo mafuriko hutokeea kila zinaponyesha mvua za mvuo. Jamii inayojikuta katika mazingira hayo inapaswa kujua ni hatua zipo za kuchukua. Mathalan ujenzi wa matuta, kuhimiza wakazi, kusakini katika maeneo ya juu ya nchi, huduma za dharura za kupambana na maradhi yanayochimbukana na ungi wa maji na kadhalika. Vivyo hivyo na ukame. Ni muhali kuweza kujua ukame anatokea lini. Hata hivyo jamii inaweza kuchukua hatua fulani ambazo zinachangia kwenye ukame kama ukataji miti kiholela. Uchimbaji wa chemichemi ni njia nyingine inayoweza kutumia hasa kuhakikisha kuwa ikiwa ukame utatokea, watu hawataathirika kutokana na kuyakosa maji ya kutumia.

Wataalam wameafikiana sasa kuwa baada ya tsunami iliyotokea lazima uwepo mfano madhubuti wa kuweza kudodosa mtikisiko wa ardhi ambao hutokeea muda kabla ya tetemeko lenyewe. Kwa njia hii watu wataweza kuonywa mapema na labda hasara iliyotokea kupunguzwa.

Maswali

- (a) Ni nini chanzo cha Tsunami? (alama 1)

.....

.....

- (b) Eleza tokeo kuu la tsunami. (alama 2)

.....

.....

- (c) Eleza hatua anazochukua binadamu kupambana na majanga ya kimaumbile.

(alama 3)

.....

.....

- (d) Mbali na majanga ya kimaumbile yaliyotajwa katika makala, taja mengine **mawili.** (alama 2)

- (e) Taja methali inayoweza kufumbata ujumbe wa kifungu hiki. (alama 2)

- (f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivytumiwa katika kifungu hiki. (alama 4)

- (i) Kuvuvumka:.....
.....
- (ii) Kutawasiri akilini:.....
.....
- (iii) Mvua za mvuo:.....
.....
- (iv) Ungi wa maji:.....
.....

2. **UFUPISHO: (ALAMA 15)**

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Ama kwa hakika tunaishi katika kipindi kizuri cha historia. Tunachanjwa tukiwa wadogo dhidi ya magonjwa hatari; magonjwa yaliyokosa tiba kwa miaka mingi iliyopita yamedhibitiwa kwa madawa ya kisasa. Yamkini tiba itapatikana siku moja kwa magonjwa sugu yaliyosalia. Lakini ingawa binadamu amejawa na matumaini siku hizi, matumaini hayo yameanza kuyeyuka polepole kwa sababu ya mauaji ya watu barabarani. Maelfu na maelfu ya watu kote duniani hufa kila mwaka au kulemazwa kutokana na ajali za barabarani.

Si ajabu kuwa na ajali nyingi siku hizi kwa sababu magari yameongezeka. Miji mingi siku hizi haikaliki kwa sababu ya wingi wa magari. Kila unapotembea mijini ni magari tu yaliyoegeshwa. Barabara nazo zimejaa magari. Isitoshe, misitu inaendelea kufyekwa ili kutengeneza barabara zaidi za kupitia magari. Kwa sababu ya ongezeko la magari, madhara yanayosababishwa na magari yazidi kuongezeka. Kwa mfano, wavunjaji wa sheria za barabarani wameongezeka na hali kadhalika ajali zinazosababishwa na uendeshaji mbaya zimeongezeka.

Labda huu ndio wakati mzuri wa kudhibiti hali ya mambo kwa kukaza sheria za uendeshaji magari. Mitihani ya udereva, yapaswa kuwa migumu zaidi ya ilivyo sasa; madereva wote wanapaswa kufanyiwa mtihani wa kuendesha gari kila baada ya miaka mitatu hivi. Umri unamruhusu kuendesha gari lolote nao wapaswa kupandishwa hadi miaka 21, na magari yote yanapaswa kufanyiwa ukaguzi kila mwaka.

Ulevi wa aina yoyote, uwe wa pombe au wa madawa, unaweza kusababisha dereva kufanya ajali. Sheria zinazohusiana na ulevi zapaswa kukazwa zaidi. Fauka ya haya, lazima kuwe na viwango vya kasi ~~katika~~ barabara zote.

Maswali

- (a) Fupisha aya mbili za ~~mwanza~~ (alama 8)

Matayarisho

Nakala safi

(b) Ni hatua zipi za kukabiliana na uvunjaji wa sheria barabarani zilizopendekezwa na mwandishi? (alama 7)

Matayarisho

Nakala safi

3. **MATUMIZI YA LUGHA**

(a) Tumia ____ ‘enye’ katika sentensi kama: (alama 2)

(i) Kivumishi:.....

(ii) Kiwakilishi:.....

(b) Andika sentensi ifuatayo katika udogo wingi. (alama 2)

Uso wake umefura kabisa na mguu wake kulemaa baada ya kuumwa na mbwa mjini.

.....
.....

(c) Taja'mfano mmoja mmoja wa sauti zifuatazo: (alama 2)

(i) Kikwamizo cha kaa kaa laini:.....

(ii) Nazali ya ufizi:.....

(d) Onyesha shamirisho kitondo kipozi na ala katika sentensi ifuatayo.

Mwana alimjengea nyanya nyumba kwa matofali. (alama 3)

.....
.....

(e) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia jedwali.

Rehema alisoma taratibu huku mwalimu akimwelekeza vizuri.

(f) Nomino “upendo” iko katika ngeli gani? (alama 1)

.....

(g) Andika kinyume cha sentensi hii:

Watoto wameombwa waanike nguo. (alama 2)

.....

(h) Kanusha sentensi ifuatayo:

Amekuja kukuona na ataondoka kesho. (alama 2)

.....

(i) Kwa kutolea mifano ya sentensi, bainisha matumizi **matatu** ya parandisi. (alama 3)

.....

.....

.....

- (j) Eleza matumizi ya kiambishi ku katika sentensi ifuatayo:
Tulimwona na kumsalimia. (alama 1)

.....
.....

- (k) Amrishwa vitenzi vifuatavyo katika umoja na wingi. (alama 2)

(i) Fa
(ii) Imba:

- (l) Andika katika kauli ya kutendeshea.
Amebatili muradi wa maji. (alama 2)

.....
.....

- (m) Bainisha aina za virai katika sentensi ifuatayo.
Wanafunzi watatu walikuwa wamechoka sana. (alama 2)

.....
.....

- (n) Ainisha vihusishi katika sentensi hii.
Ng'ombe watatu kwa saba ndio wamechinjwa hadi sasa. (alama 2)

.....
.....

- (o) Andika kwa msemo halisi.
Tajiri alishangaa kuwa niliweza kumbeba mzigoto huo peke yangu.

.....
.....

- (p) Bainisha aina za vitenzi katika sentensi hii.
Keroro alikuwa akienda kwake usiku. (alama 2)

.....
.....

- (q) Bainisha aina za nomino zilizopigiwa mstari katika sentensi hii.
Kucheka kwa Bwana Kehongo kulionyesha raha baada ya kuionja asali. (alama 4)

.....
.....

- (r) Andika maana tatu za sentensi ifuatayo.
Mwaliko huo ulitushtua. (alama 3)

.....
.....

4. ISIMU JAMII (ALAMA 10)

(a) Kwa nini watu nchini Kenya hufanya makosa ya kisarufi wanapozungumza?

(alama 4)

.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....

(b) Fafanua sifa **sita** zinazotambulisha sajili ya kituo cha polisi.

(alama 6)

.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....